# Serikali yapiga marufuku taarifa zake kwenye mitandao binafsi

**Na Selemani Nzaro, Arusha**

SERIKALI imepiga marufuku matumizi ya mitandao binafsi zikiwemo baruapepe, WhatsApp, Instagram, You Tube, Facebook kutuma nyaraka na taarifa za serikali.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete alitangaza amri hiyo wakati akifunga kikaokazi cha sita cha Serikali Mtandao kwenye Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) jijini Arusha jana.

Ridhiwani aliwaomba watumishi wote wa umma kuendelea kuiamini mifumo ya mawasiliano serikalini ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa sababu ni imara, salama na inayoleta tija kwa mawasiliano yote ya serikali.

Alisema kuna watumishi wa umma ambao bado wanatumia njia na mitandao binafsi kutuma na kupokea taarifa na nyaraka mbalimbali za serikali, na kusisitiza kuwa hayo ni matumizi mabaya ya mifumo ya mawasiliano serikalini.

"Ni marufuku kuanzia leo kwa watumishi wote wa umma kutumia mitandao isiyo rasmi kutuma na kupokea nyaraka za serikali, kwa sababu hilo ni jambo la hatari na linasababisha nyaraka za serikali kuvuja na kuonekana mitaani," alisema Ridhiwani.

Alieleza kusikitishwa na kitendo cha watumishi wa umma kuendelea kuteswa na mikopo ya kausha damu wakati utaratibu wote wa mikopo salama unapatikana katika mifumo ya mawasiliano serikalini.

Alisema ni jambo la ajabu kuona watumishi wakilalamikia mikopo ya kausha damu, wakati serikali imewawekea mifumo inayowahakikishia kutotapeliwa na kupata mikopo inayofuata taratibu za ukopeshaji zinazotambuliwa na serikali.

"Watumishi wanatakiwa kutumia mifumo ya Tehama ambayo inayaleta mashirika yote pamoja na taasisi za fedha pamoja kuomba mikopo, kwa sababu ndio sehemu wanaweza kupata mikopo bila usumbufu wowote na kwa riba nafuu," alisema Ridhiwani.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Benedict Ndomba alisema kikaokazi hicho kimeshirikisha wadau zaidi ya 1,300 kutoka sekta za umma na binafsi na kwamba mada 14 ziliwasilishwa.

Ndomba alisema kutokana na taasisi mbalimbali za umma kutekeleza vyema miradi ya Tehama, eGA imeamua kuwapa tuzo ili iwe motisha kwao waendelee kufanya vizuri pamoja na kukuza weledi katika utendaji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dk Damas Ndumbaro alisema Tanzania imepata mafanikio Afrika katika eneo la Serikali Mtandao na kwamba kwa dunia ya leo, ni lazima kuwekeza katika Tehama ili Tanzania isonge mbele.

Dk Ndumbaro alisema kutokana na kazi nzuri ya eGA, kamati ya bunge inatambua mafanikio ya taifa na kwamba eGA imefanikiwa kuunganisha mifumo ya mawasiliano serikalini.

"Bunge ni mnufaika mzuri wa Serikali Mtandao, kwa sababu halitumii tena karatasi katika kuwasiliana na badala yake kwa sasa kila kitu kinafanyika mtandaoni," alisema Dk Ndumbaro.

Aidha, alisema kutokana na kazi kubwa iliyofanywa na eGA, muda mwingi wa wabunge umeokolewa na kwamba gharama kubwa iliyokuwa ikitumiwa na bunge kuchapa karatasi sasa imeokolewa.

Awali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Arusha, Toba Nguvila alisema mifumo ya Tehama imeongeza uwazi na uwajibikaji serikalini.

## SAUTI ZA WANANCHI BAADA YA UCHAGUZI UCHAGUZI MKUU 2025



"NAJIVUNIA Tanzania nchi yangu naipenda, mimi pamoja na Watanzania wenzangu, tunapaswa kulinda amani na utulivu kwa nguvu zote. Tuepuke kuingiza udini katika nchi yetu kwa sababu ni sumu isiyokuwa na tiba. Mataifa yaliyoingiza udini hadi leo unawatesa, tushikamane tuepuke udini na ukabila," **Mkazi wa Magole, Ilala mkoani Dar es Salaam, Frank Joseph.**



"BABA wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alituachia taifa imara lenye mshikamano na umoja. Ni aibu kwetu wajukuu zake kuibomoa nchi kwa wiki moja iliyojengwa kwa miaka zaidi ya 60. Watanzania tukatae kutumiwa kuiharibu nchi yetu wenyewe," **Mkazi wa Kijiji Cha Lwami, Mwanga mkoani Kilimanjaro, Athumani Mkwizu.**



"TUNAPASWA kujivunia kwamba ushindani wa kisiasa leo unatokana na sera na ajenda za maendeleo. Wakati wengi wetu tunasema tunapenda amani. Lazima tulinde umoja wetu kwa sababu amani ndio msingi wa ustawi na maendeleo ya taifa," **Mjasiriamali wa Temeke mkoani Dar es Salaam, Saidi Gulu**

# TRA yazionya bandari kavu

**Na Tatu Mwakabana**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imesema itawachukulia hatua za kisheria wamiliki wa kampuni za bandari kavu zinazochochea ukwepaji wa malipo ya ushuru wa forodha.

Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuph Mwenda alitoa onyo hilo alipofanya kikaokazi na wamiliki wa kampuni hizo mkoani Dar es Salaam jana.

"Nataka mfanye kazi saa 24, baadhi ya ICD ambazo zinachochea ukwepaji wa kodi au mazingira hayo, tutawachukulia hatua za kisheria," alisema Mwenda.

Aidha, alisema lengo la mkutano huo ni kujadiliana namna ya kuboresha utendaji na kuimarisha ushirikiano kati yao ili kuongeza ufanisi katika sekta hiyo.

"TRA tunawathamini na tutaendelea kuwapa ushirikiano katika kuongeza ufanisi," alisema Mwenda.

Alisema idara ya forodha na TRA hawawezi kufanya kazi zao kwa ufanisi kama bandari kavu hazitatimiza wajibu wao wa kulinda usalama wa bidhaa ambazo haziruhusiwi kuingia nchini.

Mwenda aliagiza wamiliki wa kampuni za bandari kavu kuweka utaratibu wa kukutana na TRA mara nne kwa mwaka ili kujadili changamoto na mafanikio ya utendaji kwa ushirikiano huo.

Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa wa TRA, Juma Hassan alisema ufanisi wa forodha unategemea ufanisi wa bandari kavu, kwa kuzingatia kuwa sekta ya bandari kavu inashusha mizigo mingi iliyopita katika Bandari ya Dar es Salaam na kuchangia asilimia kubwa ya Pato la Taifa.

"Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa miezi sita idara ya forodha ilitakiwa kukusanya Shilingi trilioni 6.8 lakini ilikusanya trilioni 6.9, ongezeko la asilimia moja na katika fedha hiyo asilimia 52 ilitokana na makusanyo ya mzigo inayopita bandari kavu," alisema.

Aidha, kwa upande wa chama cha wamiliki wa bandari kavu waliomba yafanyike maboresho kwenye mifumo kukabiliana na changamoto kubwa wanazokutana nazo kwenye utendaji wao.

Changamoto hizo ni pamoja na utolewaji wa leseni ya biashara kwa mwaka mmoja, muda ambao hautoshelezi upande wa mifumo ya ubebaji wa mizigo na kunasa kwa magari ndani ya bandari.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira na Mahusiano, Deus Sangu akizungumza kwenye kikao cha uhusiano na Makamu Mwenyekiti wa Pili wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) ambaye pia ni Askofu wa Kanisa la Mennonite Tanzania, Nelson Kisare (kushoto) alipowatembelea ofisini kwao Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu).

# Wasichana balehe 123,489 wanufaika

**Na Yohana Shida, Geita**

MRADI wa Uwezeshaji Wasichana Balehe Kuendelea na Masomo (KAGIS) umefanikiwa kusaidia takribani watu 123,489 katika mikoa ya Geita na Kigoma kwa miaka mitano ya utekelezaji.

Mradi wa KAGIS umetekelezwa chini ya usimamizi wa Shirika la Plan International pamoja na washirika wake ambao ni RAFIKI SDA na Shirika la WPC kwa ufadhili wa serikali ya Canada.

Mkurugenzi Mkazi wa Plan International Tanzania, Jane Sembuche alitoa taarifa hiyo jana katika hafla ya kufunga mradi wa KAGIS iliyofanyika katika Ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Geita.

Sembuche alisema miongoni mwa wanufaika hao ni wasichana, wavulana, wazazi, walezi, walimu na jamii ambao wameshiriki kwa dhamira thabiti na kufanya bidii ya kufikia mbadiliko.

Alisema ili kusaidia wasichana balehe kuhitimu masomo na kufikia malengo, KAGIS imewajengea wasichana stadi za maisha na kuwezesha uchumi wa kaya kupitia vikundi akiba na mikopo.

Alisema kupitia ustahimilivu wa kaya, mradi wa KAGIS umefanikiwa kuwanufaisha wanawake 6,000 kupitia vikundi vya akiba na mikopo pamoja na kuwezesha wasichana 7,000 kubaki shule.

"Mradi umeonesha matokeo makubwa katika mwitikio wa kijinsia kwa shule za msingi na sekondari kutoka kiwango cha awali cha asilimia 25 hadi asilimia 66 mwishoni mwa mradi," alisema. Aliongeza: "Haya ni matokeo ya mifumo bora ya ulinzi wa watoto, kuzuia ukatili wa kijinsia shuleni, kuwepo kwa maeneo salama kwa wasichana na kuimarika kwa uwajibikaji katika ngazi ya shule."

Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela alisema KAGIS imeunga mkono juhudi za serikali kuimarisha sekta ya elimu wasichana balehe kusalia shule.

Shigela alipongeza ufadhili wa serikali ya Canada katika mradi wa KAGIS, huku akieleza kuwa hayo ni matokeo ya ushirikiano thabiti wa kidiplomasia baina ya Tanzania na serikali ya Canada.

Balozi wa Canada nchini Tanzania, Emily Burns alisema Canada inatambua umuhimu wa elimu, hasa kwa watoto wa kike.